

**HOTUBA YA MHE. MAMA SALMA KIKWETE AKIZUNGUMZA NA
WANAFUNZI WA KITUO CHA KAZI ZA AMALI-VITONGOJI, NA SKULI
YA SEKONDARI YA FIDEL CASTRO, TAREHE 13 MEI, 2010.**

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba,

Mhe. Waziri ya Elimu na Mafunzo ya Amali,

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya

Mhe. Mwenyekiti wa CCM Mkoa,

Mkuu wa kituo cha Kazi za Amali Vitongoji

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kusini Pemba,

Waheshimiwa wabunge wamajimboa

Waheshimiwa Wabunge Viti Maalum,

Mkuu wa Skuli ya Fidel Castro,

Waheshimiwa madiwani na Wawakilishi,

Viongozi wa Chama na Serikali,

Walimu na wanafunzi, Mabibi na Mabwana,

Asalaam Aleykum!

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa

Rehema, kwa kutuwezesha sote kujumuika wakati huu hapa Kituo cha Kazi za Amali - Vitongoji.

Kabla ya kuendelea naomba niwafikishie ujumbe kutoka kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu Jakaya Mrisho Kikwete. Anawasalimu sana na anawapongeza watendaji wote wa sekta ya mafunzo kwa namna mnavyojitahidi kuyaboresha mafunzo haya kwa manufaa ya wanafunzi wetu na taifa letu kwa ujumla.

Ndugu wananchi

Nimefurahi sana kupata fursa hii ya kuwatembelea na kuzungumza wanajumuia wote wa Kituo cha Kazi za Amali – Vitongoji, na wale wa skuli ya Fidel Castro ambao tumejumuika nao hapa.

Ninafurahi pia kuzungumza nanyi kwani hii ni fursa pekee ya kuwapa maneno machache ya kuwatia nguvu.

Kazi za Amali ni umuhimu sana kwa vijana wetu. Kwani sekta hii muhimu inayotengeneza raslimali watu katika fani mbali mbali zikiwemo ufundi umeme, kompyuta, useremala, ufundi Magari, uashi, na ufundi bomba. Vijana muitumie vizuri fursa hii mliyoipata kwani baadae mtajikomboa kwa vile mmepata stadi za kiufundi zitakazo wapa ajira yenye manufaa makubwa kwenu.

Mhe. Mkuu wa Mkoa, wapendwa Walimu na Wanafunzi,

Kabla sijaendelea, ningependa niwafahamishe kidogo juu ya taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA). Taasisi hii ambayo mimi ni Mwenyekiti inajihusisha na utoaji wa fursa za elimu ya sekondari kwa watoto wa Kike, Afya ya mama na mtoto, Uwezesaji wanawake kiuchumi, na huduma kwa watoto yatima.

Katika elimu, tumeweza kutoa fursa ya elimu ya sekondari kwa wanafunzi zaidi ya 300 wanaotoka Tanzania Bara na Visiwani.

Mhe. Mkuu wa Mkoa, wapendwa Walimu na Wanafunzi,

Ni ukweli usiopingika kuwa **ELIMU** ndiyo **MKOMBOZI** wa maisha yetu. Hivyo ni wajibu wetu kuwasaidia wanafunzi waweze kupata elimu bora. Hapa tuna wanafunzi wa Fidel castro, shule iliyoanza siku nyingi. Hii ni ishara kuwa, tangu zamani wazee wetu walitambua umuhimu wa elimu na ndio maana shule hizo zilijengwa.

Natambua changamoto nyingi zinazowakabili katika kutoa elimu na mafunzo ya Kazi za Amali kama zilivyoainishwa na tulivyozisikia kwenye risala iliyosomwa. Ninatambua kuwa Serikali imepanga na kuweka mikakati imara ya kuboresha utoaji wa elimu hapa pemba, na ndio maana Chuo hiki cha Kazi za Amali kimejengwa ili kuwapa fursa waliokosa nafasi za kuendelea na masomo. Pia mikakati hiyo imelenga kuongeza skuli, vifaa vya kufundishia, vitabu vya wanafunzi na mengine mengi.

Hii yote ni jitihada za kuboresha elimu ambayo sote tunatambua kuwa ni muhimu sana.

Kwa mantiki hiyo basi, wadau wote tunapaswa kuvuta subira huku tukiongeza jitihada zinazolenga kuboresha utoaji wa elimu.

Wapendwa wanafunzi

Kwa upande wenu nawasisitiza muwe makini na masomo yenu. Epukeni na mambo yote yanaweza kuwaangusha kitaaluma, mathalan uzembe, utoro na suala la mimba kwa walio masomoni au mafunzoni. Jiwekeeni malengo ya makubwa kitaaluma, ili msiishie kufuzu katika ngazi hii ya mafunzo, na sekondari bali, mfaulu na mpate sifa zitakazowawezesha kuendelea na kozi za mafunzo zaidi kwa ngazi ya elimu ya juu na hata ngazi ya vyuo vikuu.

Mhe. Mkuu wa Mkoa, Ndugu Viongozi, Mabibi na Mabwana,

Nimalizie kwa kuwakumbusha wazazi na walezi kuwasaidia vijana wetu kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kujisomea wanaporudi nyumbani na wakati wa likizo.

Baada ya kusema hayo, niwashukuru tena kwa mapokezi mazuri na ukarimu mlionionesha!. Nawatakia kila lakheri *na Mungu awabariki*

Ahsanteni kwa kunisikiliza!